

1013/1
KISWAHILI, KARATASI YA KWANZA
MWIGO
MARCH 2019
MUDA : SAA MBILI

MAAGIZO

1. *Mtihani huu una sehemu nne muhimu: Insha, Ufahamu, Matumizi ya lugha na Sajili za lugha. Fuata maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.*
2. *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hii kwa lugha ya Kiswahili.*

SEHEMU	SWALI	UPEO	TUZO
1	1	20	
2	2	20	
3	3	50	
4	4	10	
JUMLA		100	

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo wa mada zifuatazo:

(alama 20)

- a) Wewe ni katibu wa kamati ya maslahi yamtaa wa Tanga. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanywa hivi karibuni, kuzungumzia swala la kuzorota kwa usalama.
- b) Ukosefu wa ajira nchini ni tatizo linaloweza kutatuliwa. Thibitisha.
- c) Mdharau mwiba huota tende
- d) Andika insha itakayomalizikia kwa: "... wenzangu, nilifikiri nilikuwa nimefika, kumbe sivyo."

1. UFAHAMU (Alama 20)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

KUKITHIRI kwa visa vya utoaji wa hongo kwa wapiga kura walioshiriki chaguzi ndogo zilizofanyika Jumatatu katika eneobunge la Malindi na Kaunti ya Kericho ni ithibati tosha kuwa ufasadi umekita mizizi nchini.

Kadhalika, visa hivyo vilidhihirisha kuwa demokrasia imedidimia na taasisi za kupambana na visa vya ufasadi zimefifia.

Mwezi uliopita, Wakenya kupitia **mitandao ya kijamii** walishtumu Rais wa Uganda Yoweri Museveni kutokana na kile walichotaja kuwa matumizi ya ‘mabavu’ kuhifadhi kiti chake baada ya kuwatishia wapinzani wake.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii pia walimkosoa Rais Uhuru Kenyatta kwa kumpongeza mwenzake wa Uganda huku wakisema aliunga mkono ukandamizaji wa demokrasia.

Lakini, visa vya uhongaji wa wapiga kura vilivyoshuhudiwa katika maeneo ya Malindi na Kericho vikitekelezwa na viongozi wa kisiasa hata wengine wakiwa wa muungano tawala wa Jubilee, ni dhihirisho tosha kuwa Wakenya hawakuwa na sababu ya kushutumu Rais Museveni.

Utumiaji wa mabavu au kununua wapiga kura ili kushinda uchaguzi ni hujuma kwa demokrasia. Baadhi ya wanasiasa pia wameripotwa kuwa wanatumia fedha zao kusafirisha watu kutoka eneo moja hadi jingine ili wajiandikishe kuwa wapiga kura na wawachague katika uchaguzi ujao. Huu pia ni ukiukaji wa misingi ya demokrasia.

Ununuaji wa wapiga kura unamaanisha **mabwanyenye** ambao wamehusishwa na sakata mbalimbali za ufasadi ndio wataendelea kushikilia nyadhifa mbalimbali za uongozi kwa kuwa wao ndio wana mabunda ya fedha za kuhonga wapiga kura.

Viongozi wanaochaguliwa baada ya kuwahonga wapiga kura hawatafanya maendeleo yoyote na badala yake, watakuwa wakihusika na wizi wa rasilimali za umma ili kupata fedha za kuwahonga watu katika uchaguzi unaofuatia. Mabwanyenye hawa wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wapiga kura wanaendelea kuzama katika lindi la umaskini ili waweze kununuliwa kwa urahisi. Sawa na Esau tuliyelezwa katika Biblia kwamba aliua urithi wake wa kuzaliwa kwa Yakobo kwa kubadilishana na chakula, maskini pia wako tayari kuuza haki yao ya kuchagua kiongozi bora kwa shilingi mia moja.

Viongozi wanaotoa hongo kwa wapiga kura kwa lengo la kushinda uchaguzi ni ishara kwamba hawana maono wala sera za mandeleo. Badala yake wanang’ang’ania **mamlaka** ili kujilimbikizia utajiri wala si kusaidia mpiga kura kujinua kimaisha.

(Taifa leo. Machi 10, 2016)

Maswali

- a) Kwa kurejelea kifungu, visa vya kutoa rushwa kwa wapiga kura vinadhihirisha nini? (Alama 3)
- b) Bainisha jinsi nne ambazo viongozi wa kisiasa wanatumia kuendeleza ukiukaji wa misingi
- c) Fafanua athari za uozo unaorejelewa katika taarifa kwa
 - (i) Viongozi (Alama 2)
 - (ii) Raia (Alama 2)
- e) Kulingana na taarifa, demokrasia imedidimia vipi? (alama 3)
- d) Thibitisha kuwa nyani haoni ngokoye katika muktadha wa makala haya (Alama 2)
- e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa (Alama 3)
 - (i) mitandao ya kijamii
 - (ii) mabwanyenye
 - iii) mamlaka

SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (alama 50)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3 a) Taja sauti zenye sifa zifutazo. (alama 4)

Kikwaruzo cha ufizi kinachoghuna / /

Kipasuo/kituo cha ufizi kisichoghuna / /

Nazali ya mdomoni inayoghuna / /

Irabu ya mbele, kati isiyoviringa / /

a) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wingi. (alama 2)

Fundi wa nguo ashoneaye juani ana cherehani.

b) Tumia kihusishi cha a - ya uhusiano kutunga sentensi katika wakati uliopita. (alama 2)

c) Tunga sentensi ukitumia ngeli ya KU-KU kama: (alama 4)

Kivumishi
Kiwakilishi.

d) Toa mfano wa neno moja lenye mofimu tegemezi. (alama 2)

e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali / visanduku. (Alama 4)

Natala ni riwaya nzuri.

f) Bainisha maana tatu tofauti za sentensi hii ikiwekewa shadda au mkazo tofauti katika neno la mwisho. (alama 3).

Waite vijana wale.

g) Andika upya kwa kufuata maagizo. (alama 2)

Unyanyapaa ulisababisha kutoroka kwake shuleni. Tumia neno lililokolezewa wino katika kauli ya kutendewa.

h) Tunga sentensi moja yenye maneno yafuatayo; (alama 3)

Amini, amani, amana.

Eleza matumizi ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari. (Alama 2)

Mvulana mtanashati ameshinda tuzo. Mtanashati yule amesoma sana.

i) Tumia kihisishi cha kiapo kutunga sentensi katika wakati ujao. (alama 2)

j) Tambua makosa mawili katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mzee Mjumbe alimwangaalia Dunia na kumfokea, “utakimbia hadi lini hawafu wee”!

4.

- a) _____ ni ugonjwa wa kukojoa damu unaotokana na maji machafu. (alama 1)
- b) Andika katika maneno. (alama 2)
- $$\sqrt{25} = 5$$
- c) Nywele zinazomea kifuani huitwa _____ ilhali _____ ni zile nywele zinazomea katika sehemu nyeti. (alama 2)
- d) Anayeendesha gari la moshi _____ (alama 1)
- e) _____ ni kitendo cha kutikisa mti ili kuangusha matunda. (alama 1)
- f) Kuku mwenye shingo bila manyoya huitwa _____ - _____ (alama 1)
- g) Utamwitaje mke wa mtoto wako? (alama 1) _____
- h) Furungu, njuga, udodi na usinga ni mapambo. Taja ni pambo lipi halilingani na mengine na ni kwa nini. (alama 2)
- i) Tunga sentensi **moja** kudhihirisha maana tofauti za neno shinda. (alama 3)
- j) Taja semi inayooana na maelezo yafuatayo;
Kuonja chakula ulichompakulia mgeni kabla ya kukila kama njia ya kumhakikishia kuwa hakiwezi kumdhuru. (alama 2)
- k) Toa methali nyingine yenye maana sawa na hii; (alama 2)
Mwomba chumvi huombea chunguche.
- l) Fumbua fumbo hili (alama 2)
Baba ako na shamba lenye umbo lifuatalo hapo chini na ambalo angependa kuwaridhisha wanawe wanne kwa masharti kwamba wakigawana, vipande vyote vitoshane na kila kipande ni lazima kiwe na umbo la shamba asilia. Onyesha jinsi wanavyoweza kufanya hivi.

SEHEMU YA NNE: SAJILI ZA LUGHA

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 10)

MTU 1: Majina yako kamili?

MTU 2: Musa Baridi.

MTU 1: Unaishi wapi?

MTU 2: Mtaa waManyatta.

MTU 1: Hebu eleza ulikuwa wapi tarehe 8/2/2019 saa tano asubuhi.

MTU 2: Siku hiyo saa hizo...

a) MTU 1 na MTU 2 wanawakilisha akina nani? (alama 2)

b) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. (alama 2)

c) Fafanua sifa zozote tatu za sajili hii. (alama 8)